# USCRI JUA HAKI ZAKO

## Mwongozo kwa Wahamiaji

Bila kujali hali ya uhamiaji, batu bote mu inchi ya Marekani bako na haki zenye zinalindwa na kuhakikishwa na Katiba. Hii mwongozo imetayarishwa kwa kujulisha batu benye habako banainchi ba Marekani kuhusu haki zao za kisheria mu hali mbalimbali wakati banakutanana na maafisa wa sheria na maafisa wa uhamiaji.

Sheria za majimbo fulani zinaweza kutofautiana. Sheria tofauti zinatumika mu vituo ya ukaguzi na wakati ya kuingia Marekani kupitia fasi rasmi za kuingilia mu inchi, sawa vile ku mipaka na ku viwanja ya ndege.

**Hii maelezo imetolewa kwa malengo ya elimu na haipashwi kutumiwa ku nafasi ya msaada wa kisheria. Kama weye ao mutu mwenye unajua anahitaji msaada wa kisheria, tafazali wasiliana na mwanasheria.**

## KAMA UNAFUNGIWA NA MAAFISA WA KUTEKELEZA SHERIA AO WA UHAMIAJI



- Usiseme atakitumoya kwa maafisa wa polisi ao maafisa wa kutekeleza sheria ao wa uhamiaji. Uko na haki ya kubakiya kimya kila wakati. Kila kitu yenye utasema inaweza kutumiwa zidi yako ku mahakama.
- Sema, “Minapenda nizungumuze na  mwanasheria.” Kuanzia pale, polisi ao afisa wa uhamiaji anapashwa acha kukuuliza maswali.
- Kama unafungiwa na po lisi,  uko na haki ya kupata mwanasheria wa bure (mwanasheria wa serikali) mu kesi za uhalifu.
- Kama unafungiwa na afisa wa uhamiaji, uko na haki ya kusaidiwa na mwanasheria kuhusu hali yako ya uhamiaji, lakini serikali haina haja ya kukupatiya mwanasheria -lomba mwanasheria mara moya.
- Lomba ukuwe na mutafsiri kama Kingereza haiko luga yenye unajisikia muzuri zaidi kuongea.



- Usisaini kitu ata moya na hauya zungumuza na mwanasheria.
- Kama unakuwa mu mikono ya ICE, wasiliana na mwanasheria wako ao mwanamemba wa jamaa mara moya. Uko na haki ya kuita ku simu kisha kufungiwa.
- Lomba kuachiliwa kwa muda na kusikilizwa kwa ajili ya kesi yako mbele ya muamuzi, hata kama ICE inasema haustahili.
- Lomba nakala za barua zako zote za uhamiaji.